

Kanuni za Maadili kwa Wauzaji wa Cargill

Ahadi yetu ya kuisaidia dunia *kustawi*

Lengo la Cargill ni kusitawisha dunia kwa njia salama inayowajibika na endelevu. Tunaelewa kuwa mifumo ya uzalishaji na ugavi inayohimili mfumo wa dunia wa chakula sharti iwe endelevu – ili iweze kusawazisha mahitaji ya leo na mahitaji ya vizazi vijavyo. Tunaweza tu kufikia malengo yetu kwa kufanya kazi kwa karibu na Wauzaji Washirika wetu. *Kanuni yetu ya Maadili kwa Wauzaji* inaeleza jinsi tunavyotarajia wakulima, wazalishaji, watengenezaji na watu wengine wafanye kazi nasi ili kufikia lengo hilo – kwa kuzingatia maadili na kuambatanana sheria zinazotumika.

Kanuni zinazotuongoza

Kanuni saba zinazoiongoza Cargill zinafuatwa na wafanyakazi wetu wote; ndizo msingi wa shughuli zetu kote ulimwenguni. Kanuni yetu ya Maadili kwa Wauzaji inawajumuisha Wauzaji Washirika wetu katika kuendeleza kanuni zizi hizi. Tunaamini kuwa ushirikiano huu wa kuhakikisha maadili na uwajibikaji ni msingi imara kwa mahusiano yanayoaminika ya kibiashara yanayoleta faida kwa kila mshirika.

---

1. Kuzingatia sheria

Tukiwa kampuni inayowajibika, tunatarajia kuwa Wauzaji Washirika wetu kote ulimwenguni wataungana nasi katika jitihada zetu za kufuata sheria.

Matarajio yetu kuwa Wauzaji Washirika Wetu ni:

- Kijua na kufuata sheria zinazowahusu na kuhusu biashara zao
- Kuzingatia masharti ya kisheria kama kanuni msingi
- Kutoa habari kwa Cargill iwapo kuna matatizo yoyote yanayohusiana na bidhaa na huduma wanazotoa—hasa matatizo ya kiafya na usalama. Kufanya hivi huisaidia Cargill kufuata kanuni zinazotumika ulimwenguni kote

2. Kufanya biashara kwa uadilifu

Tunataka mahusiano ya kibiashara yanayofuata misingi ya uaminifu, uwazi na uwajibikaji wa kila mhusika.

Matarajio yetu kuwa Wauzaji Washirika Wetu ni:

- Kushindana kwa njia ya usawa na kufuata maadili ya biashara
- ya Cargill

  Kutotoa wala kukubali hongo, kiinua mgongo, zawadi au ukarimu usiofaa au marupurupu haramu kuhusiana na biashara na Cargill
- Kuepuka mgongano wowote wa kimaslahi unaohusiana na maslahi ya kifedha au mipango mingine isiyokubalika kati yako na wafanyakazi wetu
- Kufanya kazi kwa kushirikiana na wauzaji wao wenyewe ili kukuza ushirikiano wa kibiashara unaolingana na sheria za Kanuni hizi

3. Kuweka rekodi sahihi na za kweli

Tunataraji Wauzaji Washirika wetu watadumisha rekodi sahihi na za kweli. Kufanya hivi kutatusaidia kutoa uamuzi bora wa kibiashara na kutoa maelezo ya kweli na yanayotolewa kwa wakati unaofaa kwa washika dau wetu.

Matarajio yetu kuwa Wauzaji Washirika Wetu ni:

- Kuweka rekodi na vitabu vinavyoonyesha miamala yote kwa njia sahihi, ya kweli na kwa wakati faafuKutumia michakato inayofaa ya ukaguzi ubora na kuzingatia kanuni kwa mambo mathalan yanayohusu bidhaa, chakula, usalama wa chakula, afya na usalama wa wafanyakazi, kazi na ajira
- Kutoa maelezo panapohitajika, kuhusu maeneo ilipo hifadhi na asili inayotambulika ya bidhaa ili kuwezesha ufuatiliaji

4. Kutimiza ahadi za kibiashara

Tunafanya kazi pamoja na Wauzaji Washirika wetu wenye ari sawa nasi ya kuunda mahusiano ya kibiashara. Hii inahitaji mawasiliano ya wazi, heshima kati ya wahusika wote na kutimiza ahadi.

Matarajio yetu kuwa Wauzaji Washirika Wetu ni:

- Kujitolea kufanya biashara kwa kuzingatia ukweli na uwazi
- Kutimiza ahadi za biashara na kuthibiti matukio yasiyotarajiwa kwa wakati unaofaa na kwa njia ya uwazi

5. Kuwashughulikia watu kwa kuzingatia utu na heshima

Tunatarajia kuwa Wauzaji Washirika wetu wataungana nasi ili kuhakikisha usalama, afya na utu wa kila mmoja aliye na kipawa na anayefanya kazi kwa bidii ili kutuwezesha kuwasilisha bidhaa na huduma zetu.

Matarajio yetu kuwa Wauzaji Washirika Wetu ni:

- Kuandaa mazingira ya kazi kuwa salama na yanazingatia kanuni za afya katika sehemu zote za kazi
- Kutojihusisha wala kukubali ulanguzi wa binadamu, ajira ya lazima au ya watoto kama ilivyoelezwa na Shirika la Kazi Duniani (ILO)
- Kuweka mazingira ya kazi yanayojumuisha watu wote na ambayo hayana unyanyasaji wala ubaguzi
- Kuzingatia haki za wafanyakazi za kujumuika na kujitetea kwa pamoja
- Kutimiza kanuni zote za malipo na hali ya kazi

6. Kulinda maelezo, mali na rasilimali za Cargill

Tunatarajia Wauzaji Washirika wetu wadumishe sifa bora ya Cargill pamoja na malezo au mali yoyote tutakayoshiriki nao.

Matarajio yetu kuwa Wauzaji Washirika Wetu ni:

- Kulinda habari yoyote ya siri ya Cargill ambayo wanaweza kuipata, ikiwa ni pamoja na hakimiliki, siri za biashara au maelezo ya kifedha
- Kuhakikisha kuwa wamelinda mali yoyote ya Cargill iliyo chini ya udhibiti wao
- Kuepuka hali yoyote ambayo huenda ukaathiri biashara zetu au sifa yetu

7. Kuwa raia mwema wa dunia

Tunawategemea Wauzaji Washirika wetu kuwa wataisaidia Cargill kulisha dunia kwa njia salama, ya uwajibikaji na endelevu.

Matarajio yetu kuwa Wauzaji Washirika Wetu ni:

- Kudumisha viwango vya juu vya ubora ili kukuza bidhaa, chakula na usalama wa lishe
- Kujitahidi kupunguza madhara ya mazingira kupitia juhudi kama vile kukomesha ukataji miti, kupunguza gesi za sumu na kutumia rasilimali kwa njia bora
- Kulinda rasilimali za maji kwa kupunguza matumizi ya maji kwenye shughuli zao, kuepuka uchafuzi kutokana na shughuli zao na kupunguza athari kwa rasilimali za maji kwa jamii zinazoishi karibu nao
- Kuheshimu kanuni ya kuomba ridhia mapema bila kushinikizwa na baada ya kupata maelezo kamili kuhusu haki za rasilimali na umiliki za jamii asili
- Kushirikiana na Cargill ili kutekeleza michakato endelevu na kutatua matatizo ili kuhakikisha uboreshaji unaodumu na kuendeleza maadili ya jamii

Lengo letu la ushirikiano unaoaminika

Ni lengo letu kuunda mahusiano yenye misingi ya kuaminiana na Wauzaji Washirika wenye maadili na wanofuata Kanuni hizi Saba za Zinazotuongoza. Tunatarajia Wauzaji Washirika wetu kushirikiana nasi kutupa maelezo, kutoa vyeti na/au ruhusa ya kufikia maelezo ya kukagua mahesabu. Iwapo kuna tatizo, kwa kawaida sisi hufanya kazi pamoja Muuzaji Mshirika wetu. Tunaweza kusaidia kutambua mbinu ambazo huenda zikasaidia kuboresha hali. Hata hivyo, iwapo tatizo haliwezi kutatuliwa au muuzaji mshirika hataki kushirikiana nasi, tuna haki ya kukatiza usirikiano wetu.

Kwa kufanya kazi kwa ukaribu na Wauzaji Washirika wetu, tunaamini kuwa tunaweza kupata mafanikio huku tukizisaidia jamii na ulimwengu kwa jumla kusitawi.

Kwa maelezo zaidi, angalia www.cargill.com/supplier-code. Ukiona ua ushuku miendendo au shughuli zozote za kibiashara ambazo unafikiri huenda zinakiuka Kanuni za Maadili kwa Wauzaji, tafadhali wasiliana moja kwa moja na Cargill. Unaweza kutoa malalamiko au kupata usaidizi kwa:

- Kuwasiliana na mwakilishi wako wa Cargill; au
- Kupiga simu kwa nambari yetu salama na iliyo wazi ya Cargill Ethics. Maelezo ya kuwasiliana na maelezo zaidi kwa zaidi ya lugha 20 yanaweza kupatikana katika https://www.cargill.com/about/ethics-open-line-en.

Kuwasiliana nasi kwa njia ya haraka husaidia kuzuia matatizo na kutatua matatizo yoyote ambayo tayari yapo. Tunashughulikia ripoti zote kwa haraka, kwa njia ya haki na kwa kuzingatia siri.

Cargill®

Helping the world *thrive*